

## **MUHTASARI WA MWENENDO WA MVUA KWA TAREHE 01–10 JULAI, 2018 NA MATARAJIO YA MVUA KWA SIKU KUMI ZA KATI ZA MWEZI JULAI (11– 20 JULAI, 2018)**

### **1.1 MUHTASARI WA MWENENDO WA VIASHIRIA NA MFUMO WA MVUA KWA TAREHE 01–10 JULAI, 2018**

Katika siku kumi za mwanzo za mwezi Julai 2018, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kaskazini mwa dunia (Azores na Siberia) iliendelea kudhoofika wakati ile iliyopo sehemu ya kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) ilikuwa imeimarika. Ukanda wa mvua (ITCZ) ulielekea kaskazini zaidi. Pamoja na kuimarika kwa mgandamizo mkubwa wa hewa wa kusini, kulikuwa na eneo lenye mgandamizo mdogo wa hewa hali iliyopelekea vipindi vya upepo mkali katika baadhi ya maeneo ya nchi. Joto la bahari katika maeneo ya kusini-magharibi mwa bahari ya Hindi lilikuwa la wastani na kusababisha kutokuwepo kwa vimbunga baharini. Upepo ulivuma kutoka kusini hadi kusini-mashariki katika maeneo mengi ya nchi. Eneo la Kusini-mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola) kuliendelea kuwepo na joto la bahari la wastani hadi juu kidogo ya wastani. Hali hii ilisababisha kupunguza kwa mifumo ya kusababisha mvua katika maeneo ya magharibi mwa nchi

### **1.2 MUHTASARI WA MWENENDO WA MVUA KWA TAREHE 01–10 JULAI, 2018**

Mwenendo wa viashiria vya hali ya hewa hapo juu vilionyesha kuimarika kwa migandamizo ya hewa iliyopo kusini hali iliyopelekea kuendelea kusogea kwa ukanda wa mvua kuelekea mbali na nchi. Uwepo wa mawimbi anga kutoka mashariki kulipelekea vipindi vya mvua nyepesi katika maeneo ya ukanda wa Pwani. Pia kulikuwa na vipindi vya upepo mkali na mawimbi makubwa katika maeneo ya Pwani

### **2.0 MATARAJIO YA HALI YA HEWA KATIKA SIKU KUMI ZA KATI KWA MWEZI JULAI (11–20 JULAI, 2018)**

#### **2.1 VIASHIRIA NA MFUMO WA MVUA KWA SIKU KUMI ZA KATI ZA JULAI (01– 20 JULAI, 2018)**

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) inatarajiwa kuendelea kudhoofika wakati ile iliyopo kusini (St. Helena na Mascarene) inatarajiwa kuendelea kuimarika. Ukanda wa mvua (ITCZ) unatarajiwa kuendelea kusogea kuelekea kaskazini hali itakayopelekea upepo kuvuma kutoka kusini hadi kusini mashariki katika maeneo mengi ya nchi. Joto la bahari la wastani hadi chini ya wastani linatarajiwa katika eneo la kusini-magharibi mwa bahari ya Hindi hali itakayoondoa uwezekano wa kutokea vimbunga katika bahari. Upepo unatarajiwa kuvuma kutoka kusini hadi kusini-mashariki hali itakayopelekea hali ya baridi katika maeneo mengi ya nchi. Eneo la Kusini-mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola) kunatarajiwa kuwa na joto la bahari la wastani hadi juu kidogo ya wastani. Hali hii itapelekea kupunguza kwa upepo uvumao kutoka kagharibi hivyo kupunguza nguvu ya mifumo isababishayo mvua katika maeneo ya magharibi mwa nchi.

2.2 MWELEKEO WA MVUA KWA SIKU KUMI ZA MWANZO ZA MWEZI JULY (11–20 JULAI, 2018)

**Kanda ya ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara):** Vipindi vya mvua zinazoambatana na ngurumo za radi katika maeneo machache.

**Nyanda za juu kaskazini-mashariki (Mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro,):** Mvua nyepesi katika maeneo machache

**Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, Pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba):** Mvua nyepesi katika maeneo machache.

**Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora):** Mawingu kiasi.

**Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida):** Mawingu kiasi.

**Nyanda za juu Kusini-magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa):** Mawingu kiasi kwa ujumla.

**Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi):** Mvua nyepesi katika maeneo machache.

**Kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma na Maeneo ya kusini mwa Morogoro):** Mawingu kiasi kwa ujumla

Imetolewana; **MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA**